# MAKAMBAKO YETU

www.makambakotc.go.tz | Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali | Halmashauri ya Mji Makambako



# JARIDA MAALUM LA MWENGE WA UHURU 2024 HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



**Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru 2024 Halmashauri ya Mji Makambako.**

**M**wenge wa Uhuru 2024 ulipokelewa katika Halmashauri ya Mji Makambako juni 21,2024 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe,ikiwa ni siku ya sita tangu Mwenge ulipowasili Mkoani Njombe.

Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Mji Makambako ulipitia Miradi 4 yenye thamani ya Mil. 308 na ulikimbizwa kilomita 79.1 katika Kata 4 kati ya 12 za Halmashauri ya Mji Makambako,ambazo ni Kata ya Lyamkena,Kitisi,Kitandililo na Mlowa.

Miradi itayopitiwa na Mwenge ni mradi wa parachichi kwa wanufaika wa TASAF katika Kata ya Lyamkena,Mradi wa mnufaika wa mkopo wa asilimia 10 kijana mwenye mahitaji maalum, Sumbuko Sanga katika Kata ya Kitisi, ujenzi wa nyumba pacha ya watumishi zahanati ya Nyamande kata ya Kitandililo na mradi wa madarasa matatu shule ya sekondari ya Kitandililo-Mbugani pamoja na kuzindua klabu ya rushwa shuleni hapo.

Mwenge wa Uhuru pia katika eneo la mapokezi ulipitia banda la uchaguzi kijiji cha Ikelu,banda la lishe katika mnyororo wa thamani wa zao la parachichi katika Mtaa wa Lyamkena.

Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024 ni Ndg. Godfrey Mzava na kauli mbiu ya Mwenge kwa Mwaka huu ni “Tunza Mazingira na shiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu”.





**Maandalizi yaendelee na wananchi wapate taarifa kamilifu za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.**

Na. Lina Sanga

Wito huo ulitolewa  na Ndg. Godfrey Mzava,kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa juni 21, 2024 katika Kijiji cha Ikelu baada ya kutembelea banda la uchaguzi ambalo ni mahususi kwa ajili ya utoaji wa elimu ya uchaguzi.

Mzava alisema kuwa, agenda ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni ya kudumu katika Mikutano na vikao vya ngazi za Halmashauri,Wilaya na maeneo mengine, hivyo viongozi wanapozungumza na wananchi waendelee kusisitiza masuala yanayohusu uchaguzi kwa kuwapa taarifa kamilifu kuhusu uchaguzi pamoja na kusisitiza amani,utulivu na usalama katika kupindi chote cha uchaguzi.

Aidha, alitoa wito kwa viongozi kushusha miongozo kwa wananchi wanayopokea kutoka Serikalini, ili waweze kupata taarifa kamilifu kuelekea kwenye uchaguzi ili kila mmoja atimize haki yake ya kikatiba na kidemokrasia kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Pia , alitoa rai kwa mratibu wa uchaguzi, Halmashauri ya Mji Makambako Ndg. Yusto Nyamle kuongeza kasi ya kuwapa wananchi taarifa sahihi za uchaguzi, ili kila mmoja ashiriki kikamilifu kwani uchaguzi huo unatoa picha ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.





**Wanufaika wa TASAF watakiwa kutorudi nyuma kiuchumi,kwa kuhakikisha wanazalisha kile wanachowezeshwa na Serikali.**

Na. Lina Sanga

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,Ndg. Godfrey Mzava amewataka wanufaika wa TASAF nchini kutorudi nyuma kiuchumi , kwa kuhakikisha wanazalisha miradi wanayopewa na Serikali kwa kutia jitihada ili kufikia malengo

.

Mzava, alitoa wito huo juni 21,2024 alipotembelea mradi wa parachichi kwa wanufaika wa TASAF katika Halmashauri ya Mji Makambako, ambao walipewa miche kumi ya parachichi kila mmoja ili kuwajengea uchumi endelevu baada ya miaka mitatu na kuboresha lishe kwenye Kaya zao.

Akizungumza na wanufaika hao ikiwa ni pamoja na Bi. Evelina Nyali, mkazi wa Mtaa wa Lyamkena,Mzava alisema kuwa lengo la Serikali ni kuona wanufaika wote wanapiga hatua kwa kuzalisha miradi ambayo wanawezeshwa ikiwa ni pamoja na parachichi,hivyo kila mnufaika ajitaidi kuongeza miche mingine kuunga mkono juhudi za Serikali.

Aliipongeza Halmashauri ya Mji Makambako kupitia idara ya Kilimo kwa usimamizi bora wa mradi huo, kwa kuwatembelea wanufaika na kuwawezesha namna bora  ya kuhudumia miche hiyo.

Kwa niaba ya wanufaika wote wa TASAF wa Halmashauri ya Mji Makambako Bi. Nyali ameishukuru Serikali kwa kumuwezesha kiuchumi na kufanikiwa kuboresha makazi,kipato cha familia na lishe kwa kupitia mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe ambao umemuwezesha kupata fedha na kuanzisha mradi wa ufugaji wa nguruwe , pamoja na mradi wa parachichi ambao baada ya miaka mitatu anatarajia kuanza kupata faida ya mradi huo na kutoa rai kwa Serikali kuwasaidia wengine wenye uhitaji ili waweze kujitegemea kwani kwa sasa yeye ana uwezo wa kuendesha maisha yake.



JARIDA MAALUM LA MWENGE.indd 7 6/28/2024 4:34:34 PM



## Miradi 4 yenye thamani ya Mil. 308 yapitiwa na Mwenge wa Uhuru 2024 Halmashauri ya Mji Makambako.

Na. Lina Sanga

**M**wenge wa Uhuru 2024 umepitia Miradi 4 yenye thamani ya Mil. 308 katika Halmashauri ya Mji Makambako ambapo kati ya miradi hiyo,miradi miwili imefunguliwa na Mwenge wa Uhuru.

Mwenge wa Uhuru 2024 ulitembelea miradi miwili ambayo ni mradi wa parachichi kwa wanufaika wa TASAF 1,825 wenye thamani ya Mil.150.7 na mradi wa mnufaika wa Mkopo wa asilimia kumi iliyokuwa ikitolewa na Halmashauri ambaye alipata mkopo wa Mil. 5.

Aidha Mwenge wa Uhuru umefungua miradi miwili ambayo ni mradi wa ujenzi wa nyumba pacha za watumishi wa Zahanati ya Kijiji cha Nyamande katika Kata ya Kitandililo yenye thamani ya Mil. 91.5 na mradi wa madarasa matatu katika shule ya sekondari Mbugani-Kitandililo, yenye thamani ya Mil. 61.4 ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali,ruzuku ya

Serikali kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2024, Ndg. Godfrey Mzava kabla ya kufungua miradi hiyo alipongeza utekelezaji wa miradi hiyo na thamani ya pesa inaonekana kama Serikali ilivyokusudia.







**Mwenge wa Uhuru waagiza vijana kupewa fursa ya mikopo,Serikali ikifungua upya dirisha la mikopo ya asilimia 10.**

Na. Lina Sanga

Mwenge wa Uhuru 2024 umeiagiza Halmashauri ya Mji Makambako kumpa kipaumbele katika utoaji wa mikopo ya asilimia 10,kijana mwenye ulemavu, Ndg. Sumbuko Sanga anayejishughulisha na kazi za ufundi selemala,katika Mtaa wa Kahawa,Kata ya Kitisi pindi Serikali itapofungua dirisha la utoaji wa mikopo hiyo.

Wito huo ulitolewa na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndg. Godfrey Mzava alipotembelea mradi wa mnufaika huyo ambaye ni mlemavu (kiziwi) katika Mtaa wa Kahawa, Kata ya Kitisi mnamo juni 21,2024.

Mzava alisema kuwa, ipo haja kwa Halmashauri kuwapa vipaumbele vijana wanaojituma kwa kufanya kazi kwa bidii kwa kuwapa mikopo ili waendelee kujiajiri na kuajiri vijana wengine,badala ya kuwapa mikopo

watu wengine waliokosa uaminifu ambao baada ya kupata mikopo wanakimbia.

Aliongeza kuwa, pindi utoaji wa mikopo hiyo utakapoanza Halmashauri imuwezeshe kijana huyo kupata mashine kubwa kwa ajili ya kazi zake ,na kumtafutia eneo kubwa la kufanyia shughuli zake ili kumuwezesha kuwa na eneo kubwa kwa ajili ya kuhifadhia samani anazotengeneza kabla ya kuchukuliwa na  mteja.

Ndg. Sumbuko Sanga, ameishukuru Serikali kwa kumuwezesha kupata mkopo wa Mil. 5 ambao umempa ajira na kumuwezesha kuajiri kijana mmoja na kuwa na ofisi ambayo inamuwezesha kupata wateja.

Aidha, kijana huyo alitoa meza moja yenye ubunifu wa kuvutia kama zawadi kwa Rais  Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ndg. Mzava alikiri kuifikisha.



# MATUKIO KATIKA PICHA














G.E.MZAVU




MBIO ZA MWENGE WA UHURU
2024
MKOA WA NJOMBE


N.H. AHMED
G.E.MZAVA




Courage





































JARIDA MAALUM LA MWENGE.indd 26 6/28/2024 4:35:44 PM


















Jarida hili limetolewa na; Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
Halmashauri ya Mji Makambako